

TOLEO LA. 06


Jarida la *Ni Magufuli Tena*

2020 - 2025

ALIAHIDI | AMETEKLEZA | APEWE TENA 5 | 5 SEPTEMBER, 2020



KAMPENI YA MAGUFULI MARA ...IMEISHA HIYO!



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**



RAIS MAGUFULI AKONGA NYOYO ZA WANANCHI MKOA WA MARA

- Atimiza Ndoto ya Mwalimu Kujenga Hospital ya Rufaa liyokwama tangu 1975
- Kuendelea Kumuenzi Baba wa Taifa kwa Vitendo
- Uwanja wa Mkendo Watapika Umati wa Watu

Na Mwandishi Wetu - **MUSOMA**

Mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli ameahidi kumuenzi Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa kukamilisha ujenzi wa Hospitali aliyoianzi-sha na kiuwezesha kutoa huduma za kibingwa ikiwemo kusafisha figo ili kuwaondolea adha wananchi kusafiri hadi Dar es Salaam.

Ameyasema hayo wakati wa mkutano wa kuomba kura uliofanyika mjini Msoma ambapo amebainisha kuwa ujenzi wa Hospitali hiyo ulikwama tangu mwaka 1975 lakini Serikali yake imejenga hospitali hiyo tayari huduma zimeanza na kuwaahidi wakazi wa mkoa wa Mara kuwa Serikali itanunua mashine maalumu ya kusafisha figo.

"Mbali na hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere tumejenga Hospitali za Wilaya 7, Vituonane vya afya, Zahanati 27 ambapo miradi yote imegharimu bilioni 25.1," ameeleza Rais Magufuli.

Kwa upande huduma za Bima ya afya Rais Magufuli amesema kuwa mfumo huo umeonesha mafanikio makubwa hivyo mipango iliyopo ni kuhakikisha huduma za bima ya afya inawafikia wataanzania wote.

Mbali na kuboresha huduma za afya katika mkoa huo, Rais Magufuli amewaeleza wakazi wa mkoa wa Mara kuwa Serikali itaujenga uwanja wa ndege wa Musoma kwa kiwango cha lami ili kurahisisha huduma za ndege katika mkoa huo.

“Tayari tumeshatangaza tenda ya kumtafuta mkandarasi atakayejenga uwanja wa ndege wa Musoma kwa kiwango cha lami na tayari shilingi bilioni 49 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi huo,” alieleza Rais Magufuli.

Rais pia ameelezea utekelezaji wa Serikali katika miradi ya maji mkoani humo ambapo amesema miradi 38 ya maji yenye thamani ya shilingi bilioni 68.4 inatekelezwa na kati ya hiyo, miradi 17 imekamilika na iliyobaki inaendelea kutekelezwa.

“Tumejengwa barabara zenye urefu wa Kilomita 283 kwa kiwango cha lami na Kilomita 1,147 kwa kiwanago cha Changarawe pamoja na madaraja makubwa sita kwa gharama ya shilingi bilioni 171.2,” anaeleza Rais Dkt. Magufuli.

Kwa upande wa Bandari ya Musoma amesema itaimarishwa katika kipindi cha miaka mitano ili meli zinazojengwa na zilizokarabatiwa na Serikali katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ziweze kutoa huduma kwa wananchi wa mkoa huo na Mataifa ya jirani.



SAMIA SULUHU HASSAN: MWAROBAINI WA MAFURIKO DAR WAPATIKANA

Na Mwandishi Wetu - DAR ES SALAAM



Adha ya mafurukokwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam sasa inakwenda kuwa historia baada ya Serikali kutenga zaidi ya shilingi bilioni 32 kwa ajili ya katika ujenzi wa mifereji kwenye maeneo ya mabonde Jijini Dar es Salaam, lengo likiwa ni kuzuia mafuriko na kuwaweka salama wakazi waishio kwenye maeneo hayo.

Hayo yamesemwa na mgombea mwenza wa nafasi ya Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) Mhe. Samia

Suluhu Hassan wakati wa mkutano wa kampeni uliofanyika katika viwanja vya shule ya msingi Tabata Jijini Dar es Salaam.

"Ndugu zangu tunatambua changamoto za miundombinu kwenye Jiji hili, na ndio maana tunajenga barabara za juu, madaraja na mifereji, Daraja la Salenda linaendelea vizuri, interchange ya ubungo tunakaribia kumaliza na tumetenga fedha zaidi ya shilingi bilioni 32 za mifereji ili kuzuia mafuriko," alisema Samia.

Akifafanua kwa kusema kuwa Serikali pia inaendelea kuimarisha miundombinu ya barabara, mifereji na madaraja Jijini humo ili kupunguza msongano wa magari ambao ulikuwa ukiathiri shughuli za kiuchumi.

Kuhusu ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Vingunguti Mhe. Samia amebainisha kuwa mchinjio hayo huiingizia Serikali pato la zaidi ya shilingi milioni 100 kwa mwezi. Maesema kuwa tayari zimetengwa shilingi bilioni 12.49 ambapo hadi kufikia Septemba 30 mwaka huu, mashine za kisasa za uchinjaji zitakuwa zimefungwa.

Kuhusu elimu Mhe. Samia alisema wametenga shilingi bilioni 44.5 kuboresha sekta hiyo kwa kujenga madarasa, ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Amezungumzia uboreshaji wa miundombinu katika sekta ya utalii ambapo Jiji hilo litajenga ukumbi mkubwa wa kisasa wa kitalii ambao utajumuisha hoteli, huku mikakati ya kutengeneza gati kwa ajili meli kubwa za kitalii ikifanywa.

Aidha, Serikali inaendelea kuboresha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na utalii kutoka shilingi bilioni 2.6 ya sasa hadi kufikia shilingi bilioni sita ifikapo mwaka 2025.

Mgombea Mwenza wa nafasi ya Urais ataendelea na kampeni zake katika mikoa mbalimbali hapa nchini kuwaomba wananchi kuchagua Serikali ya Awamu ya Tano kwa kipindi cha pili cha miaka mitano.



MAJALIWA AANIKA MAFANIKIO YA SERIKALI JIJI LA ARUSHA

- Asema Serikali imetekeleza Miradi ya Shilingi Bil. 577. 53 Jijini Arusha

Na Mwandishi Maalum



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa amesema Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli imetoa shilingi bilioni 577.53 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya afya, elimu, maji na miundombinu ya barabara jijini Arusha. Mhe. Majaliwa ameyasema hayo leo Septemba 5, 2020 alipohutubia mkutano wa kampeni uliofanika katika uwanja wa Relini jijini Arusha, baada ya kumuomba kura Rais Dkt. John Pombe Magufuli na mgombea ubunge jimbo la Arusha, Mrisho Gambo na

wagombea udiwani wa CCM.

Waziri Mkuu amesema kati ya fedha hizo shilingi bilioni 1.3 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Arusha ambapo jengo la wagonjwa ya nje (OPD) limekamilika na ujenzi wa jengo la akina mama unaendelea. "Jumla ya shilingi bilioni 1.5 zimetolewa kwa Jiji la Arusha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya vya Muriet, Kaloleni na Moshono ambapo ujenzi wake umekamilika na wananchi wanaendelea kupatiwa huduma," ameeleza Mhe. Majaliwa.

Waziri Mkuu amesema mbali na ujenzi wa hospitali na vituo vya afya, pia Serikali imetoa shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ununuzi wa dawa na vifaa tiba kwa kipindi cha 2015/2016-2019/2020 katika jiji la Arusha, upatikanaji wa dawa umefikia asilimia 98.

Amesema Serikali imetoa shilingi bilioni 2.14 kwa ajili ya kugharamia shughuli za ukarabati, utawala, michezo, mitihani na posho kwa maofisa elimu kata na walimu wakuu katika shule za msingi 48 jijini Arusha. "Shilingi bilioni 4.68 zimetolewa katika shule za sekondari 29 kwa ajili ya fidia ya ada, chakula kwa shule za bweni na posho ya madaraka kwa Wakuu wa Shule."

Pia, Waziri Mkuu amesema shilingi bilioni 1.03 zimetolewa na Serikali kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu ya madarasa na vyoo kwa shule mbalimbali za msingi jijini Arusha ikiwemo Olasiti, Daraja II, Oloirien na Sokoni.\

Akizungumzia kuhusu shule za sekondari, Waziri Mkuu amesema Serikali imetoa shilingi bilioni 4.68 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya madarasa, mabweni, vyoo na majengo ya utawala ikiwemo shule za Suye, Muriet, Lemara, Sorenyi, Arusha na Korona.

"Jiji la Arusha linakabiliwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama, hivyo Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 520 kwa ajili ya mradi wa majisafi jiji la Arusha ambao utahudumia Jiji lote la Arusha. Utekelezaji wake umefikia asilimia 52," ameeleza.

Amesema shilingi bilioni 38.4 zimetolewa kupitia TARURA katika kipindi cha 2015/2016 - 2019/2020 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami na madaraja kwa jiji la Arusha ikiwemo ujenzi wa barabara ya Oljoro - Muriet yenye urefu wa Kilometa 2.8. Barabara nyingine ni za Kisongo Bypass Kilometa 3.4, barabara ya Sokoine -Muriet Meidimu urefu wa Kilometa 8.5, barabara ya Njiro Kilometa 2.8, barabara ya Ngarenaro Kilometa 4.1 na ujenzi wa barabara ya Sombetini Kilometa mbili.

"Barabara ya Arusha - Holili/Taveta. Ujenzi wa sehemu ya barabara kutoka Sakina hadi Tengeru, Km14.1 na ujenzi wa barabara ya mchepuko wa kusini (Southern-bypass), Km 42.41 ambazo zinajengwa na TANROADS (Wakala wa Barabara Tanzania) zitahudumia Jiji lote la Arusha na Halmashauri za Wilaya Arusha na Meru."

Mhe. Majaliwa ametumia fursa hiyo kuwasihi wananchi wa Arusha kumchagua Rais Dkt. Magufuli kwa kuwa ana uwezo mkubwa wa kusimamia mambo yanayowagusa wananchi na ametekeleza vyema Ilani ya CCM ya mwaka 2015 kwa vitendo na sasa anakuja na Ilani mpya iliyosheheni mambo mengi ya maendeleo.

Waziri Mkuu ameongeza kuwa katika kipindi cha miaka mitano watanzania wakiwemo wakazi wa mkoa huo wamenufaika kutokana na miradi mbalimbali ya kimkakati ambayo imejengwa nchini ikiwemo ufufuaji wa usafiri wa treni ya Dar es Salaam hadi Arusha ambao ulikuwa umesimama kwa takribani miaka 30.

CCM ARUSHA YAZIDI KUKUBALIKA UCHAGUZI MKUU 2020

- Wananchi Watoa Ushuhuda wa Mafanikio ya Serikali
- Wadai Wamechoshwa na Ahadi Hewa za CHADEMA

Na Mwandishi Wetu - **ARUSHA**



Jiji la Arusha limezizima na kujikuta shughuli zote zikisimama kutokana kile kinachotajwa kuwa ni mvuto na hamasa waliyopata wananchi wa Jiji hilo kwa Chama cha Mapinduzi (CCM) kutokana nakazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Maelfu ya wananchi wa rika zote wamejitokeza katika viwanja vya Relini kuungana na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa katika mkutano wake wa hadhara kumwomba kura Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli anayegombea nafasi hiyo kwa kipindi cha pili baada ya kufanya kazi kubwa ya kuleta mageuzi ya kiuchumi.

Tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani mwaka 2015, wakazi wa Jiji la Arusha wameonesha kuzichoka siasa za upinzani hususan CHADEMA baada ya Serikali inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli kufanya mageuzi makubwa katika Jiji hilo.

Jiji la Arusha limezizima na kujikuta shughuli zote zikisimama kutokana kile kinachotajwa kuwa ni mvuto na hamasa waliyopata wananchi wa Jiji hilo kwa Chama cha Mapinduzi (CCM) kutokana nakazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Maelfu ya wananchi wa rika zote wamejitokeza katika viwanja vya Relini kuungana na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa katika mkutano wake wa hadhara kumwomba kura Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli anayegombea nafasi hiyo kwa kipindi cha pili baada ya kufanya kazi kubwa ya kuleta mageuzi ya kiuchumi.

Tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani mwaka 2015, wakazi wa Jiji la Arusha wameonesha kuzichoka siasa za upinzani hususan CHADEMA baada ya Serikali inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli kufanya mageuzi makubwa katika Jiji hilo.

Baadhi ya Jiji la Arusha hakika limeonesha kwa limeelewa kazi alizofanya mgombea wa Chama cha Mapinduzi katika Jiji hilo ikiwemo utekeleji kwa mradi mkubwa wa maji wenye thamani ya shilingi zaidi ya bilioni 600, maboresho katika sekta ya afya, ujenzi wa barabara za lami katika jiji hilo, taa, miundombinu wezeshi na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kupitia mikopo ya riba nafuu kwa wakinamama, vijana na walemavu.

Baadhi ya Wananchi waliohojiwa akiwemo Bw. Onesmo Masawe (34) amesema kuwa kila mkazi wa Arusha ameguswa na utekelezaji wa Rais Magufuli kupitia miradi ya maendeleo lakini zaidi ni namna mamia ya vijana, wanawake na walemavu walivyonufaika kwa kupatiwa mikopo na vitendea kazi ikiwemo bodaboda. Naye Edna Palangyo (47) wa Kaloleni Arusha, amebainisha kuwa kama Kijana hana budi kumuunga mkono Rais Magufuli na mgombea Ubunge wa Jimbo la Arusha, Mrisho Gambo kutokana na utendaji uliotukuka na kuwasaidia wanyonge hasa wamachinga kama yeye ambapo miaka ya nyuma walikuwa wakinyanyaswa na mgambo wa Jiji.

“Arusha ya sasa ina sifa zote za kuongozwa na Mbunge kutoka CCM kwa sababu ndio Chama pekee chenye kutoa matumaini. Kwa miaka 10 tumemchagua Lema lakini amekuwa akilumbana na Serikali tu na kuzurura kwenye majimbo ya wengine kufanya migomo badala ya kutuletea maendeleo. Safari hii asahau kabisa kura zetu, tumechoka. Tunamchagua Magufuri na Gambo,” anaeleza Edna.

Mzee Michael Lekumok Laizer (63) wa Kwa Mrombo ambaye nae alifika viwanja vya Relini kumsikiliza Mhe. Majaliwa anesema kuwa katika maisha yake hajawahi kuona mabadiliko makubwa yakitokea katika mkoa wa Arusha kama wakati wa uongozi wa Rais Magufuli.

“Sasa hivi sisi huu Arusha tunafurahia maisha kwa sababu tunapata huduma zote za jamii kama hospitali na zahanati zimeongezeka na mabarabara kuzunguka mji mzima ni ya lami tu, sio kama zamani kulikuwa na vumbi,” anaeleza Mzee Laizer huku akiomba Mungu ampe umri mrefu aendelee kuiona Arusha ikibadilika.



MAMA MARIA NYERERE ATINGA GHAFLA KATIKA MKUTANO WA MAGUFULI MUSOMA

- Asema Yeye ni Kichwa Kingine Kinachomuongezea Nguvu Mgombea Urais

Na Mwandishi Wetu - **Musoma -MARA**

Mjane wa Baba wa Taifa, Mama Maria Nyerere ameshindwa kujizua na kuamua kufunga safari kutoka Kijijini Mwitongo, Butiama hadi Musoma mjini kwa ajili ya kumuombea kura Mgombea Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Dkt. John Pombe Magufuli.

Ujio wa Mama Maria Nyerere ulitangazwa na Katibu Mwenezi wa CCM, Humphrey Polepole na kuamsha shangwe kubwa kutoka kwa maelfu ya wananchi kutoka Musoma Mjini na Wilaya za jirani ambao walifika kushuhudia kampeni za Rais Maagufuli katika Uwanja wa Mkendo.

Katika mkutano huo, Mama Maria Nyerere alisimama kuwasalimia wananchi na kumnadi Rais Magufuli ili wananchi wa Mkoa wa Mara na watanzania wote wampi-gie kura za ndio Rais Magufuli katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, 2020.



“Mimi ni kichwa kingine kilichokuja kuongeza nguvu kwa Rais Magufuli, najua wengi mtampigia kura lakini mimi nimekuja kuongeza kura nyingine”. “Mimi nina kura moja ila ninawaomba tuungane pamoja tumpe kiongozi wetu aweze kumaliza yale waliyoyapanga”, alisem Mama Maria Nyerere.

Akihutubia wananchi waliofika kumsikiliza, Rais Magufuli amemshukuru Mama Maria Nyerere kwa upendo mkubwa alionao kufika katika mkutano huo yeye pamoja na watoto wake, Makongoro pamoja na Madaraka.

Rais Magufuli pia aliwamwagia sifa watoto wa Baba wa Taifa kwa kwa kuendeleza demokrasia nchini ikiwemo kushiriki kingang’anyiro cha kugombea nafasi ya Ubunge katika Jimbo la Butiama ambapo Makongoro na Madaraka walishiriki.

Kabla ya Mama Maria kuongea, Watoto wawili wa Hayati Baba wa Taifa, Madaraka Nyerere na Makongoro Nyerere walipewa fursa ya kuongea ambapo walimuelezea Rais Magufuli kama ni kiongozi mchapakazi na ameimarisha umoja na mshikamano pamoja na kusimamia misingi aliyoiishi Hayati Baba wa Taifa.



KALI ZA MAGUFULI MKOANI MARA SEPTEMBER 5, 2020

- 1.** TUNAJENGA UWANJA WA NDEGE WA KISASA HAPA MUSOMA KWA GHARAMA YA ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 49 ILI NDEGE ZOTE ZIWE ZINATUA HAPA IKIWEMO BOMBARDIER. FIDIA IMESHALIPWA KWA WANANCHI AMBAO MAENEO YAO YAMETWALIWA KADIRI YA MAHITAJI YA UJENZI.
- 2.** TUTAIMARISHA BANDARI YA MUSOMA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITANO IJAYO ILI MELI TULIZOKARABATI NA TUNAZOJENGA ZIFIKE HAPA KUTOA HUDUMA KAMA ILIVYOKUWA AZMA YA HAYATI BABA WA TAIFA, MWALIMU NYERERE.
- 3.** TUTAIWEZESHA HOSPITALI YA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE KUTOA HUDUMA ZA KUSAFISHA FIGO NA PIA TUNAJIPANGA KUTOA HUDUMA YA BIMA YA AFYA KWA WANANCHI WOTE ILI KUMUENZI NA KUTAMBUA MCHANGO WA HAYATI BABA WA TAIFA.
- 4.** TUMEJENGA KWA KIWANGO CHA LAMI BARABARA ZENYE UREFU WA KILOMETA 283 NA MADARAJA SITA KWA SHILINGI BILIONI 171.2. PIA TUTAKAMILISHA UJENZI WA BARABARA ZA LAMI ZILIZOBAKI HAPA MUSOMA IKIWEMO YA MUSOMA MJINI HADI MSEKELA.
- 5.** TUMETUMIA SHILLING BILIONI 25 KUTEKELEZA MIRADI YA SEKTA YA AFYA IKIWEMO UJENZI WA HOSPITALI ZA WILAYA, ZAHANATI, VITUO VYA AFYA, - VIFAA TIBA NA VITENDANISHI.

MGOMBEA MWENZA CHAUMA ATAKA WANANCHI WACHAGUE KIONGOZI MZALENDO

Na Mwandishi Wetu - **DAR ES SALAAM**



Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMA) kimezindua rasmi kampeni kwa nafazi za Rais, Wabunge na Madiwani leo Jijini Dar es Salaam huku Mgombea Mwenza wa Chama hicho, Mohamed Masoud Rashid akiwataka wataanzania kumchagua Rais mzalendo na mwenye uchungu na rasilimali za nchi.

“Tusichague bora Kiongozi kwa kuwa huyo hana uchungu na nchi wala rasilimali zake na maslahi nchi. Badala yake atatanguliza mbele maslahi yake na ya waliomtu-ma.

“Kiongozi wa sasa amefanya makubwa ambayo kila anayebisha anafanya makusudi kwa sababu za siasa tu, lakini kila mwenye macho haambiwi tazama,” alimalizia Mgombea Mwenza, Bw. Rashid. Kauli hiyo ya Mgombea Mwenza wa CHAUMA ime-tafsiriwa na baadhi ya wananchi kuwa inamgusa moja kwa moja Mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Dkt. John Pombe Magufuli kutokana na uzalendo aliouonesha kwa Tanzania.

“Mimi kwa mtazamo wangu Bw. Rashid hakuwa wazi tu labda kwa sababu za kisiasa lakini unaona anamlenga Rais Magufuli ambaye katika awamu kwanza ya uongozi wake amefanya mambo yaliyoshindikana kwa miaka mingi ikiwemo uzalendo aliouonesha katika sekta ya madini,” John Maganga, Mfanyabiashara wa soko la Tan-dale.

WASEMAVYO WANANCHI KUHUSU UCHAGUZI MKUU 2020



“wakweli huyu baba, hatujui cha kumpa kufutia upendo alionao kwetu sisi wananchi wa hali ya chini, kwa sasa tunafanya biashara zetu ndogondogo bila kero, tutampatia kura huyu baba aendelee kutulinda maana hatuajui akija mwingine kama atakuwa kama yeye,” alisema Annastazia Anyomwisye, mkazi wa Solwa.

Aika Mboya, mkazi wa Kahama, yeye ameeleza kufurahishwa na kauli za Dokta Magufuli, kuwa ni za kweli na hazina unafiki kwakuwa Rais Magufuli.

“Hakikawanawake tutampigia kura Magufuli, kwakuwa tunajua wapi alikotoa, ametufikisha wapi na tunaona kabisa anakotupeleka, alisema, Aika Mboya.

Kwa upande wake Kijana Emmanuel Shija, mkazi wa Kishapu, amesema, Rais Magufuli, ataendelea kukaa mioyoni mwa vijana wengi wa Mkoa wa Shinyanga, kufuati mikopo isiyo na riba wanaopatiwa na Halmashauri kufuatia Sheria inayoelekeza kila halmashauri nchini kutenga asilimia kumi ya mapato yake kwaajili ya wanawakem-Vijana na watu wenye Ulemvu.

“Tuko vijana zaidi ya arobaini katika kikundi chetu cha “Vijana Tuuungane”, tume-patiwa mkopo usio na riba na halmashauri yetu na kila mmoja kanunua bodaboda yake na sasa tunajipatia riziki na tunaendesha maisha yetu, kwakweli tutampa JPM kura pasi na shaka yoyote, alimalizia,” Emmanuel Shija.

Wakati huo Mgombea huyo wa Urais kupitia Chama cha Mapinduzi, ameahidi kuzishighulikia kero zote za wananchi wa Shinyanga ikiwemo barabara na sakata la wastaafu wa SHIRECU kutolipwa mafao na mishahara yao.

Mgombea huyo wa CCM, anayetarajiwa kuendelea na kampeni ya Chama hicho hapo kesho, amewaomba wananchi wa Shinyanga, kumpa ridhaa yeye, Wabunge na Madiwani, aongoze muhula mwingine wa miaka mitano ili wapate fursa nzuri ya kumpima kwa miaka kumi.

Jarida la Ni Magufuli Tena

2020 - 2025



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**